



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

CHUO CHA MAFUNZO YA UFUGAJI NYUKI - TABORA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na.BTI/AJIRA/VOL.I/35

Tarehe: 10/06/2026

## TANGAZO LA AJIRA YA KUJITOLEA

NAFASI ZA AJIRA ZA KUJITOLEA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUGAJI  
NYUKI – TABORA

Mkuu wa Chuo cha Mafuzo ya Ufugaji Nyuki – Tabora anatangaza nafasi za ajira ya kujitolea kwa wahitimu wote wa Kitanzania wenye sifa kama zinavyoainishwa kulingana na kada husika.

### 1. Mtunza Ghala la Chuo (Store keeper) nafasi 1

#### 1.1 SIFA ZA KIJANA WA KUJITOLEA;

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi umri wa miaka 35; Awe Mhitimu wa elimu ya Cheti cha ngazi ya Astashahada, Stashahada au Shahada kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali;
- ii. Awe Mmiliki halali wa vyeti vya kitaaluma;
- iii. Awe na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Umma;
- iv. Awe na barua ya Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Serikali za Mitaa;
- v. Awe na utayari wa kujitolea katika eneo husika;
- vi. Awe hajawahi kuhukumiwa na Mahakama kwa makosa ya jinai au nidhamu;
- vii. Awe na mwenendo na tabia njema inayokubalika na jamii; na
- viii. Awe hajawahi kuajiriwa katika Taasisi yoyote ya Umma tangu alipohitimu masomo.

#### 1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kutunza Ghala na vifaa vyake
- ii. Kusimamia na kuratibu kazi za Ghala
- iii. Kutunza taarifa za vifaa vinavyoingia na kutoa ghalani.

## **2. Msaidizi Ufugaji Nyuki nafasi 1**

### **2.1 SIFA ZA KIJANA WA KUJITOLEA;**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi umri wa miaka 35;
- ii. Awe Mhitimu wa elimu ya Cheti cha ngazi ya Astashahada, Stashahada au Shahada kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali;
- iii. Awe Mmiliki halali wa vyeti vya kitaaluma;
- iv. Awe na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Umma;
- v. Awe na barua ya Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Serikali za Mitaa;
- vi. Awe na utayari wa kujitolea katika eneo husika;
- vii. Awe hajawahi kuhukumiwa na Mahakama kwa makosa ya jinai au nidhamu;
- viii. Awe na mwenendo na tabia njema inayokubalika na jamii; na
- ix. Awe hajawahi kuajiriwa katika Taasisi yoyote ya Umma tangu alipohitimu masomo.

### **2.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kusimamia na kutunza manzuki za Nyuki
- ii. Kushiriki katika uvunaji wa mazao ya Nyuki
- iii. Kuchukua taarifa za uzalishaji na maendeleo ya makundi ya Nyuki na kuwasilisha kwa msimamizi wake
- iv. Kupanda na kutunza bustani ya maua yatumikayo na nyuki
- v. Kushirikiana na wakufunzi katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo
- vi. Kufanya majukumu mengine atakayopangiwa na mkuu wake.

## **3 Fundi sanifu umeme nafasi 1**

### **3.1 SIFA ZA KIJANA WA KUJITOLEA;**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi umri wa miaka 35; Awe Mhitimu wa elimu ya Cheti cha ngazi ya Astashahada, Stashahada au Shahada kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali;
- ii. Awe Mmiliki halali wa vyeti vya kitaaluma;
- iii. Awe na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Umma;
- iv. Awe na barua ya Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Serikali za Mitaa;
- v. Awe na utayari wa kujitolea katika eneo husika;
- vi. Awe hajawahi kuhukumiwa na Mahakama kwa makosa ya jinai au nidhamu;
- vii. Awe na mwenendo na tabia njema inayokubalika na jamii; na
- viii. Awe hajawahi kuajiriwa katika Taasisi yoyote ya Umma tangu alipohitimu masomo.

### 3.2 MAJUKUMU YA KAZI


- i. Kukagua na kuripoti kasoro za kiufundi za mifumo ya umeme (Electrical Faults);
- ii. Kushughulikia kasoro ndogo ndogo za kiufundi za mifumo ya umeme;
- iii. Kufanya usanifu na matengenezo madodgo madogo ya umeme;
- iv. Kufuatilia na kuhakiki ankara za umeme; na
- v. Kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

### UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote ya tumwe kwa:

MKUU WA CHUO,  
CHUO CHA MAFUNZO YA UFUGAJI NYUKI – TABORA,  
S.L.P 62,  
TABORA.

Mwisho wa kutuma maombi kwa nafasi zote ni tarehe 22 Juni, 2026  
saa 9:30 alasili.



H.A.Nyamaliza

Kny: MKUU WA CHUO